**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# KITUO CHA TAIFA CHA UHIMILISHAJI (NAIC) USA RIVER

## MAONO

Kuboresha uzalishaji wa mifugo kwa kutumia mbegu bora za madume ili kukuza kipato na kutokomeza umaskini kwa mfugaji

## DHIMA

Kutafuta madume bora kokote duniani ya kuzalisha mbegu bora na kuzisambaza kupitia wahimilishaji kulingana na mahitaji ya wafugaji kwa lengo la kuboresha koo-safu za mifugo yao ili kuongeza uzalishaji wa nyama na maziwa nchini.

## MIKAKATI

Tunathamini Mahitaji ya wafugaji kwa kutoa ushauri wa matumizi ya mbegu bora kulingana na mazingira pamoja na matakwa ya mfugaji. Kuimarisha shughuli za uhimilishaji kwa kutafuta mbegu bora zaidi na kutunza kumbukumbu za uhimilishaji kwa ufuatiliaji wa karibu. Kuwa na maabara yenye uwezo wa kukusanya mbegu kutoka kwa madume bora, kuzihifadhi na kuzisambaza. Kuimarisha shughuli za uhimilishaji na kuwafikia wafugaji wengi iwezekanavyo kupitia vituo vya kanda na wahimilishaji walioenea nchi nzima. Kuwa na mfumo wa kutunza kumbukumbu za uhimilishaji ili kuwezesha upatikanaji wa kizazi bora. Kufundisha wataalamu wa uhimilishaji na kusambaza vifaa vya uhimilishaji.

## WASILIANA NASI


S.L.P 7141
ARUSHA - TANZANIA
Simu: +255 27 2541056/ 0757835393
Namba ya Ofisi: +255 32971456/732971456
Fax: +255 272541058/ 2541042
Tovuti: https://www.naic.go.tz
Email: info@naicmifugo.or.tz

## NITAJUAJE KAMA NG'OMBE ANAHITAJI KUHIMILISHWA? (DALILI ZA JOTO)

1. Anahangaika na kuwapanda wenzake
2. Anasimama na kutulia anapopandwa na wenzake.
3. Hupunguza kiasi cha maziwa kwa siku hiyo.
4. Maeneo ya nje ya uke huvimba na kutoa ute ukeni
5. Kupiga kalele za mara kwa mara
6. Anapunguza kiasi cha chakula kwa siku hiyo.

## MUDA MUAFAKA WA KUHIMILSHA NG'OMBE ALIYEONEKANA KUWA NA DALILI ZA JOTO

Dalili kuu inayoonyesha kuwa ng'ombe yupo kwenye joto ni kusimama wakati akipandwa. Hivyo ng'ombe akionekana kuwa kwenye joto asubuhi atapandishwa jioni. Na kama ataonekana jioni atapandishwa asubuhi siku inayofuata. Ubora wa ng'ombe wa maziwa ni wingi wa maziwa kwa gharama nafuu. Unaweza kumhimlisha ng'ombe wa kienyeji upate chotara atakayeto maziwa mengi na kustahimili mazingira husika.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.Lishe bora ya mnyama
2.Kinga dhidi ya magonjwa ya mifugo
3.Mahali pazuri na salama pa kulala/kuishi mnyama (Mabanda bora na uzio)
4.Maelekezo ya wataalamu juu ya dlili za joto na muda muafaka wa kuhimilisha.

## UPATIKANAJI WA HUDUMA YA UHIMILISHAJI

Kiini cha huduma hii nchini Tanzania ni Kituo cha Taifa Cha Uzalishaji mifugo kwa Chupa (National Artificial Insemination Centre) kilichoko Usa River, kilomita 18 kutoka Arusha mjini kwenye barabara iendayo Moshi. Kituo kina majukumu yaliyoorodheshwa hapo chini, lakini hufanya kazi pamoja na wadau wake kote nchini.

## MBEGU ZA AINA YA NG'OMBE (BREEDS) WANAOPATIKANA NAIC USA RIVER



### FRIESIAN

Ni ng'ombe wa maziwa, anauzito wa kilo 400-600 majike na kilo 600 - 1,000 kwa madume. Hukua haraka na kufikia kupandwa akiwa na kilo 240 katika umri wa miezi 12 hadi 18. Huzaa ndama mwenye wastani wa kilo 35.




## AYRSHIRE

Ni ng'ombe wa maziwa, anauzito wa kilo 400 -500 kwa majike na kilo 500 - 600 kwa madume. Hukua haraka na kufikia uzito wa kupandwa akiwa na kilo 230 katika umri wa miezi 18 hadi 24. Hutoa maziwa mazito ikilinganishwa na maziwa ya Friesian.



## JERSEY

Ni ng'ombe wa maziwa ,ana uzito kilo 300 - 400 kwa jike na kilo 400 - 500 kwa dume. Ana maziwa mazito yenye rangi ya njano na yanamafuta mengi.Hustahimili mazingira na magonjwa kuliko ng'ombe wengine wa kigeni.



## SIMMENTAL

Ni ng'ombe wa nyama na maziwa, Ana wastani wa uzito kilo 900 kwa jike na kilo 1,300 kwa dume. Anakuwa haraka na anauwezo wa kuongeza kilo 1.44 kwa siku akiwa katika matunzo mazuri. Pia ana ngozi nene inayomfanya astahimili Magonjwa yanayoenezwa na kupe.



## FLECKVIEH

Ni ng'ombe wa, nyama na maziwa. Ana wastani wa uzito wa kilo 600 (jike) na kilo 900 (dume). Nyama ni asilimia 57.2 ya uzito wake anakua haraka na ana uwezo wa kuongeza kilo 1.44 kwa siku akiwa katika hali nzuri ya matunzo. Uzao wa kwanza anaweza kutoa maziwa lita 6,000 na kwa uzao unaofuata mpaka lita 10,000. Maziwa yake yana kiasi cha protini 3.7% na mafuta 4.2%

Ana ngozi nene inayomfanya kustahimili magonjwa yanayoenezwa na kupe.



## SAHIWAL

Ni ng'ombe wa nyama na maziwa, ana uzito wa kilo 400-500 kwa jike na kilo 700-900 kwa dume. Hutoa maziwa lita 8-10 kwa siku yenye mafuta 4.5% pia ana chuchu nene hivyo ni rahisi kukamuliwa ana uvumilivu wa magonjwa, anaweza kufugwa sehemu yoyote hapa nchini.



## BORAN

Ni ng'ombe wa nyama,ana wastani wa uzito wa kilo 500 (jike) na kilo 900 (dume). Nyama ni Asilimia 57 ya uzito wake. Ana uwezo wa kuishi sehemu yoyote hapa nchini,uwezo mkubwa wa kuzaliana na hustahimili magonjwa yanayosambazwa na kupe.



## BONSMARA

Ni ng'ombe wa nyama, ana wastani wa uzito wa kilo 600 kwa jike na kilo 800 kwa dume. Ana uwezo mkubwa wa kuzaa kila mwaka,ndama huzaliwa akiwa na uzito mdogo na kukua haraka baada ya kuzaliwa na pia hustahimili mazingira.



Huzar 417 Jersey

Ubora wa ng'ombe wa maziwa ni wingi wa maziwa kwa gharama nafuu.Unaweza kumuhimilisha ng'ombe wa kienyeji upate chotara atakayetoa maziwa mengi na kustahimili mazingira.

## Huduma za Uhimilishaji

Uhimilishaji ni njia ya kumtungisha mimba mnyama jike kwa kuweka mbegu za dume kwenye kizazi bila wanyama (dume na jike) kukutana kimwili.

## KWA NINI NJIA HII INATUMIKA NA INAPENDEKEZWA?

Ni njia pekee ambayo inabadilisha uzao wa wanyama kwa haraka zaidi. Hii ina maanisha kwamba, kama mfugaji ana ng'ombe wa kienyeji ni rahisi kumtungisha mimba ya dume wa kisasa wa aina inayofaa kwenye eneo lake na hivyo kupata chotara ambaye atayamudu mazingira husika.

Ni njia sahihi ya kuzuia kuenea kwa magonjwa ya kizazi kama vile Ugonjwa wa kutupa mimba (Brucellosis)., Vibriosis, Leptospirosis na Trichomoniasis. Magonjwa haya yanaenezwa kwa ngo'mbe dume aliyeathirika kumpanda ng'ombe jike. Magonjwa haya huleta hasara kubwa kwa wafugaji hasa ya kukosa uzao wa ng'ombe kwa wakati uliotarajiwa.

Mfugaji anaepuka gharama na hatari za kufuga madume. Madume wa ng'ombe wa kisasa huwa ni wakali na wakubwa, wanahitaji malishao mengi na uangalifu mkubwa wakati wa kumfuga.

Kurahisisha uchaguzi wa dume linalotakiwa kuwekwa kama dume la mbegu. Kwa kutumia njia ya uzalishaji kwa chupa wazalishaji (breeders) wanarahisishiwa kumchagua dume (replacement bull) kwa sababu mbegu za madume zinakuwa zimeshatumika kwa ngombe wengi kuliko kwa kutumia njia ya kawaida.

### Kutunza kumbukumbu sahihi za uzalishaji

Kuzalisha majike mengi kwa kutumia dume mmoja. Dume mmoja katika uhai wake anaweza kutoa mbegu zaidi ya dozi laki moja (100,000), hata kama akifa atakuwa anaendelea kutumika..

Mfugaji hahitaji kumswaga ngombe wake kwenda kwa dume. Hii inaweza kuhatarisha usalama wa ng'ombe wake, yeye mwenyewe pia kuharibu mazingira.

Ni rahisi mfugaji kuchagua aina ya ng'ombe anayemtaka kwa ng'ombe wake.



Dume wa NAIC wa ina ya Simmental anayeitwa Vet (502) wanafaa kwa nyama na maziwa




**NAIC USA RIVER**

Nakukaribisha mwananchi mpenda mapinduzi ya kilimo na ufugaji kuitumia huduma hii upate koo bora za ng'ombe kwa gharama nafuu.

Mbegu za madume bora waliochaguliwa kwa kuzingatia; ubora na ustahimilivu wa hali ya hewa, aina (breeds) utakazopenda za ng'ombe na gharama za utunzaji NAIC Usa River ni jibu lako na ni kwa ajili yako.




Ng'ombe wa kienyeji anaweza kuhimilishwa kwa kutumia mbegu za Boran au nyingine ili kupata chotara atakae faa kwa Nyama au Maziwa.